

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Tele: +255 026 2322761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: info@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge
S.L.P. 941
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkutano wa Tisa wa Bunge unatarajiwa kuanza siku ya Jumanne tarehe 7 Novemba 2017 na kumalizika tarehe 17 Novemba 2017 Mjini Dodoma. Mkutano huu utajadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupitisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa Fedha 2018/2019. Kwa mujibu wa Kanuni ya 94 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kwa kujadili na kuishauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa

Shughuli nyingine zitakazofanyika katika Mkutano huo ni kama ifuatavyo:-

1.0 KIAPO CHA UAMINIFU

Kutakuwa na Kiapo cha Uaminifu kwa Mhe. Janet Masaburi ambaye ameteuliwa na Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.0 MASWALI

Katika Mkutano huu wa Tisa, wastani wa maswali 125 ya Kawaida yanatarajiwa kuulizwa na Wabunge. Aidha, wastani wa Maswali 16 ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yanatarajiwa kuulizwa tarehe 9 Novemba na 16 Novemba, 2017.

3.0 MISWADA YA SERIKALI

Bunge pia linatarajia kupitisha Miswada Minne (4) ya Sheria ambayo itasomwa kwa hatua zake zote. Miswada hiyo ni:-

- (a) Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa Mwaka 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017*);
- (b) Muswada wa Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania wa Mwaka 2017 (*The National Shipping Agencies Bill, 2017*); na
- (c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2017*].
- (d) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017. {*The Drugs Control and Enforcement (Amendments), Bill, 2017*}

Ratiba yote ya Mkutano wa Bunge inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.parliament.go.tz.

Imetolewa na:

Katibu wa Bunge
Ofisi ya Bunge
DODOMA

06 Novemba, 2017.